IDADI WIANI YA KUKU KATIKA BANDA

- Ili uweze kufuga kuku wa nyama na kuwafanya wakue na kufikia uzito mzuri katika kipindi cha kuwauza, zingatia nafasi unayowapatia kua ni toshelezi.
- Kuku wanaopewa nafasi toshelezi huwa na ukuaji mzuri,hivyo zingatia idadi ya kuku wako na ukubwa wa banda.
- Idadi wiani ya kuku katika banda inaweza kutofautiana katika baadhi ya maeneo hasa maeneo yenye joto la juu mfano Dar es salaam na maeneo yenye baridi kama njombe
- Zingatia idadi wiani kwa kufuatisha jedwali hapa chini

IDADI YA KUKU 1M²	KANDA
10 - 15	MIKOA YA BARIDI
8 - 10	MIKOA JOTO

Katika mahesabu ya ukubwa wa banda zingatia pia nafasi inayochukuliwa na vyombo na maji.

UPANGAJI WA KUKU KATIKA MADARAJA (GRADING)

- Kuku hutakiwa kutengwa kulingana na namna ya ukuaji wao hasa wakilinganishwa katika uzito wao
- Angalau kuanzia siku ya kumi angalia namna kuku wako wanavyokua kwa kutofautiana, yaani wadogo na wakubwa
- Hivyo weka utaratibu wa kuwatenga katika makundi linganifu kutokana na uzito wao, hasa waweze kutengwa kwa kuangalia muonekano wao. Wadogo wakae sehemu tofauti na wakubwa

UTUMIAJI WA MARANDA

- Katika ufugaji wa kuku wa nyama,matumizi ya maranda ni muhimu sana.
- Maranda ya aina mbalimbali yanaweza kutumika ukilinganisha na upatikanaji wake katika eneo husika
- Kwa watumiaji wa maranda ya mbao hakikisha yanakua na kina angalau kuanzia sentimeta 5 na watumiaji wa Maranda ya mpunga yawe na kina kuanzia sentimeta 10 na kuendelea
- Weka maranda toshelezi ili uweze kuyageuza geuza na kukaa kwa muda mrefu zaidi bila ya kuyabadilisha.

Falcon Animal Feed inatoa huduma bora kwa wateja wake wakati wote ikiwemo chakula chenye ubora, Huduma za wataalam na kusikiliza maoni ya wateja wake.

Wasiliana Nasi Kupitia:

Mobile:	+255 658 531 010
Instagram:	Falcon_Animal_FeedsTanzania
Youtube:	Falcon Animal Feeds Tanzania
Facebook:	Falcon Happychicks Tanzania
Twitter:	Falcon Animal Feeds Tanzania
Website:	www.faf.co.tz
Email :	Marketing@faf.co.tz

Falcon

UFUGAJI BORA WA KUKU WA NYAMA





ULISHAJI WA CHAKULA

- Chakula na maji kinatakiwa kuwekwa katika sehemu ya kulelea vifaranga kabla ya kupokea vifaranga
- Vifaranga wanatakiwa kupata chakula mapema ili kupata uzito mzuri na kusaidia ukuaji wa mifumo ya mwili kama , mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na mfumo wa kinga za mwili.
- Fanya ukaguzi katika mfuko wa chakula wa vifaranga sehemu ya shingo ndani ya masaa 4 ili kuhakikisha kama wamekula chakula
- Weka vyombo toshelezi vya maji na chakula katika banda

Umri		Idadi ya vyombo			
		Chakula		Maji	
Siku	0 - 7	Chick plate	3	Drinker	3
	8 - 14	Feeder	3	Drinker	3
	14 - 20	Feeder	3	Drinker	3
	21 - 28	Feeder	4	Drinker	4

- Pia zingatia ulishaji wa masaa 24 kwa kuku wa nyama ,yaani wapatiwe mwanga na chakula wakati wote



- Kuku wa nyama (Broiler)wanatakiwa kupewa chakula kulingana na mahitaji yao
- Lisha Kuku wako wa nyama kwa kufuatisha mtiririko ufuatao

UMRI (SIKU)	AINA YA CHAKULA
0 - 11	Starter Crumble
12 - 18	Grower Crumble
19 - 24	Finisher Pellet

ZINGATIA

Mfumo wa ulishaji vyakula hivi kutoka Falcon umezingatia mahitaji ya wafugaji wa kuku wa nyama wanaofuga kuku kwa siku 24-30.



CHANJO

Katika kuwakinga kuku na magonjwa mbalimbali hasa yasiyo na tiba maalum,chanjo ni sehemu muhimu katika ufugaji

Kwa kuku wa nyama zingatia mtiririko ufuatao wa utoaji wa chanjo.

UMRI (SIKU)	AINA YA CHANJO
7	KIDERI (NEWCASTLE)
14	GUMBORO
21	KIDERI (NEWCASTLE)
28	GUMBORO

ZINGATIA

Siku ya utoaji wa chanjo tumia utaratibu wa kuwanyima maji angalau masaa matatu,lengo likiwa ni kuwafanya wawe na kiu ili waje kunywa maji ya chanjo kwa usahihi.

Hakikisha unanunua chanjo katika duka linalozingatia utunzaji wa chanjo katika nyuzi joto zinazotakiwa.

Hakikisha kuku wako wote wanapata chanjo siku ya utoaji wa chanjo.